# Erik Gartzke

# SURA YA 2: Uhuru wa Uchumi na Amani

Utangulizi

Kwa kuwepo kwa vita katika Mashariki ya Kati na kushamiri kwa mashambulizi ya kigaidi katika maeneo kuanzia viwanja vya ndege vikubwa hadi eneo la maduka, inafaa tujikumbushe kuwa sehemu kubwa ya dunia iko katika hali nzuri ya amani kubwa. Hakika, nchi zilizoendelea hazijapigana tangu Vita Kuu vya Pili ya Dunia. Amani hii siyo ya kawaida kwa kuwa mataifa yenye nguvu kihistoria yalikuwa katika vita vya mara kwa mara. Hata kabla ya wakati wa Thucydides, serikali zilitumia mali kupata maeneo zaidi na kutawala mambo ya jirani zao. Kwa kuelewa sababu kwamba nchi zenye nguvu za leo hazina migogoro sana kama waliowatangulia ni vigumu kudumisha amani na kupanua zaidi manufaa yake. Sera zilibashiri kuhusu uhusiano usio sahihi baina ya demokrasia na amani; kwa mfano, zinaelekea kusababisha matatizo mengi kama wanavyoyatatua.

Nadharia za kimapokeo zenye mtazamo usiojifunga zina mikondo miwili ya kuelezea amani, mmoja unaolenga aina na shughuli za serikali, mwingine kuhusu masoko huria na raslimali binafsi. Ya kwanza inaonekana zaidi katika maandishi ya Immanuel Kant, imevuta usikivu mkubwa kutoka kwa wafunzi wa siasa za kimataifa katika mwongo uliopita. Kant alikosea alivyodai kuwa jamhuri sio za vita sana kama aina nyingine za serikali, badala yake watafiti wamegundua kwamba nchi za kidemokrasia hazina tabia ya kupigana wenyewe kwa wenyewe, na haziko tayari kwa ujumla kutumia nguvu. “Amani hii ya kidemokrasia” imepigwa marufuku kisheria kwa ugunduzi kwamba demokrasia zinazoendelea zinaelekea kuwa za kivita kama udikteta unaoendelea. Maelezo yaliyopo yanayohusu juhudi zenye amani za taratibu, taasisi za kidemokrasia au kanuni za uwazi lazima zipambane kuelezea kwa nini mafanikio ni sharti la amani.

Uchumi wa kisiasa wa mtazamo usiojifunga hauna tofauti hizo. Wasomi, kama vile Montesquieu, Adam Smith, Richard Cobden, Norman Angell, Na Richard Resecrance wamekisia kwa muda mrefu kwamba soko huria lina nguvu kwa serikali huru kutoka kwenye matarajio yanayoonekana ya vita vya mara kwa mara. Ubepari unahimiza ushirikiano miongoni mwa nchi kwa kutengeneza mazingira yanayoifanya vita isiruhusiwe au isiyokuwa ya lazima. Masoko huria ni eneo lingine la ushindani miongoni mwa nchi mbalimbali, mara nyingi migogoro

ni midogo isiyohitaji utumiaji wa nguvu za kijeshi. Mageuzi ya bishara yaliyowezeshwa na uhuru wa uchumi yalipelekea pia katika mabadiliko ya masuala ya kimataifa. uvamizi unakuwa ghali na usio na faida. Utajiri katika uchumi wa kisasa ni mgumu sana "kuiba" kwa kutumia nguvu kuliko ilivyokuwa kwa jamii za kilimo na za viwanda. "Amani ya Kibepari" imekwenda na uthibitisho upo sasa kwa ajili ya kuanzisha uhusiano imara zaidi baina ya uhuru wa uchumi na kupunguza migogoro. Ninatumia kielelezo cha uhuru wa uchumi kilichotengenezwa na Gwartney na Lawson na uchambuzi mwingi wa takwimu kuonyesha kwamba masoko huria yanaelekea kuhimiza amani. Aidha ninatathmini vipengele kadhaa ambavyo mara kwa mara vimedhaniwa kuzifanya nchi zipigane. Uhuru wa uchumi ni mojawapo ya vipengele adimu ambavyo kwa kawaida vinazuia migogoro miongoni mwa mataifa.

Demokrasia inafaa kwa sababu nyingi lakini sera zinazohimiza, au hata zinazotafuta kuweka, serikali ya uwakilishi hazielekei kuchangia moja kwa moja katika amani ya kimataifa. kama matokeo yaliyoripotiwa hapa yalivyo wazi, masoko huria na si demokrasia, yana athari kubwa kwa tabia ya nchi hadi kufikia vurugu za kijeshi. Sanasana, demokrasia, inaweza kupunguza migogoro tu miongoni mwa nchi zilizoendelea kiviwanda. Nchi zinazoendelea hazinufaiki na amani ya kidemokrasia. Hasa katika majimbo yanayotawaliwa na serikali za kiautokratiki, uanzishwaji wa demokrasia unaweza kuwa na athari ndogo za mara moja katika ushirikiano wa kimataifa. Vivyo hivyo, utafiti mkubwa unaonyesha kwamba serikali ya kidemokrasia ni imara tu inapochanganywa na viwango vya hali ya juu vya maendeleo ya kiuchumi. Katika kutenganisha, sera zilizobuniwa kwa ajili ya kuzifanya nchi zinazoendelea kuwa za kidemokrasia haziwezi kuthibitisha ama uimara wa kisiasa wala amani ya kimataifa. Kwa kuwa mafanikio ni ya lazima kwa ajili ya kuwa na demokrasia imara na inayotosha kuleta amani, sera ya nje iliyo bora ni ile ambayo inaendeleza na kukuza ubepari.

Usuli

Wanafunzi wa uchumi wa siasa wa kimataifa wamehoji kwa muda mrefu kwamba masoko ya dunia yanaendeleza urafiki wa duniani. Cobden aliita biashara "utatuzi mkubwa ambao kama ugunduzi wa ufadhili wa tiba, utasaidia kukinga afya na kwa ajili ya kuokoa ustaarabu wa mataifa yote ya dunia" (1903:36). Kant aliandika kuwa ipo siku ari ya biashara, ambayo hailinganishwi na vita, itashinda katika kila nchi" (1975:32). Mill alidai kwamba "Ni biashara ambayo kwa haraka sana inaifanya biashara kutokufaa, kwa kuimarisha na kuzidisha maslahi binafsi ambayo huupinga kiasili" (1902: 390). Bila shaka tatizo, ni kwamba Mill alikosea. Vita vingi na migogoro midogomidogo vinasimama baina ya msimamo wa kutegemea mazuri wa sasa na wa zamani wa wachumi wa siasa ya msimamo wa kupendelea mabadiliko wa karne ya kumi na tisa. Walipungukiwa na nini? Walielewa nini kwa usahihi? Wana ushahidi gani kwamba msingi wa dira yao una utambuzi wenye uhalali na kudumu?

Mawazo yanapungua na kufuatana na matukio ya sasa. Madai kwamba ubepari unaweza kuzifanya nchi kuwa na vita kidogo yanakuwepo kwa urahisi wakati masoko ni mengi na hakuna vita. Wanasiasa weledi na wasomi wa karne ya kumi na tisa walijumuisha uhusiano baina ya masoko huria na amani ya kimataifa, hatimaye kuiona Ulaya ikigawanyika mwaka 1914.

Vilevile, ni rahisi kutazama dunia kama za Hobbersian kwa ujumla wakati migogoro ya kiuchumi na kisiasa inapojitokeza. Wasomi wanaangalia mambo kama yalivyo kama vile Kenneth Waltz na John Mearsheimer wakati wa Vita Baridi walishikilia kwamba uhusiano wa uchumi wa dunia haukudhuru sana uendeshaji wa masuala ya nchi, licha ya uthibitisho kwamba mataifa huru na ya viwanda ya dunia hayakuwa ya kivita sana. Uelewa madhubuti wa uhusiano wa kimataifa – bila ya kuzungumzia utafutaji wa amani duniani – unadai kwamba nadharia
ni zaidi ya muhtasari wa mtindo wa kisomi. Duniani ni mahali pa makelele. Mara nyingi, kubuni yatakayotokea kutokana na matukio ya sasa kunatupotosha. Hakika, inaelekea zaidi kwamba uhusiano baina ya uhuru wa uchumi na amani sio halisi lakini badala ya uwezekano wa tukio la kijamii na kukabiliwa njia mbalimbali za kupelekea katika vita. Kwa utumiaji wa uchambuzi wa takwimu kwa siasa za dunia, tunaweza kwenda zaidi ya mgongano wa nadharia zinazojirudia zinazothibitishwa tu na mfululizo wa visa.

Hapa, ninatoa uthibitisho kwamba uchumi huru unachangia kushuka kwa migogoro miongoni mwa nchi. Kwanza, hata hivyo, ninahitaji kuufanya kuwa wa kisasa mtazamo wa vita wa siasa – uchumi wa jadi. Mapokeo ya amani ya kibepari ni tajiri lakini wenye msingi mbovu katika utambuzi muhimu kuhusu kwa nini nchi zinapigana. Uelewa kuhusu kwa nini nchi zinapigana. Uelewa mzuri wa jinsi masoko huria yanavyookoa nchi huru kuhusu umuhimu wa kufanya vita unaweza kusaidia kuimarisha na ikiwezekana kuendeleza amani miongoni mwa nchi za kibepari zilizoendelea.

## Uhuru wa Kiuchumi na Vita vya Dunia

Norman Angell (1933), mfuasi mkubwa wa shule yenye mtazamo usiojifunga na iliyopata Tuzo ya Amani ya Nobeli kwa kazi ya uandishi na mwanasias. Anabainisha michakato miwili inayokusudiwa kupunguza maombi ya uvamizi miongoni mwa nchi zilizoendelea. Kwanza, maendeleo yanapelekea kwenye mabadiliko katika uzalishaji ambayo yanafanya mashambulizi na uvamizi visiwe na faida.

> Wakati wa robo ya mwisho ya karne ya kumi, Anlaf the Viking alikuja mara tatu Essex – na kila safari alifanya kitu kizuri: meli zake, kwa idadi 90, zilizotolewa kwenye mlango mpana zilizosheheni mahindi, na ngozi za wanyama, na nguo nzuri kutoka kwenye nyumba za watawa…. Mtiifu kwa amri ya kukumbuka kwamba nguvu zilizoko nyuma hazijabadilika, nimejaribu kuwafikiria Waingereza, sasa kwa kuwa hivi sasa wana udhibiti mkamilifu, kurudisha ukamilifu karne kumi baadaye: wanamaji wetu wakipakia sehemu nzuri ya mali zetu za biashara kwa utajiri wa bidhaa za kilimo na viwanda za rasi ya Scandinavia (Angell, 1933: 103).

Hakika, ilikuwa inaonekana kama upumbavu kumfikiria mwanamaji Mwingereza kama Marauding Vikings. Mambo yalikuwa yamebadilika ilipofikia karne ya ishirini na bado ndani ya mwongo wa uchapishaji wa toleo la pili la The Great Illusion, Uingereza ililinda Iceland[1] na karibu ivamie Norway (Kersaudy, 1990)[2], Ujerumani ilikalia Denmark na Norway (Ziemke, 1990), na Finland iliingizwa kwenye vita na Urusi (Engle na wenzake, 1992). Sweden pekee

ilibakia na uhuru wake na kutokufungamana na upande wowote.

Inachukua juhudi kidogo tu kuwafikiria Hitler, Massolini, na Tojo katika dhima ya Vikings. Nguvu za mhimili zilichangia itikadi ambayo ilikuwa na kumbukumbu wakati ambao uhimizaji wa nguvu za nchi, ulimaanisha upanuaji wa eneo (Weinberg, 1994; Cassels, 2003)3 Bado, wakati Vita Kuu vya Pili ya Dunia vingeweza kuonekana kama “jambo baya zaidi,” inawezekana kuhoji kwamba maendeleo yanazuia migogoro katika matukio fulani. Tangu mwanzo, malengo ya awali ya mihimili ya nchi yalikuwa nchi maskini kuhusu ukingo wa uchumi wa Ulaya. Vita na Ulaya Magharibi ilifikiriwa kwa sababu za kimkakati, kuzitisha Ufaransa na Uingereza, zisichukue raslimali (Weimberg, 1994). Kwa nini Hitler – mfano wa kila mtu wa ukatili – alifuatilia majimbo maskini ya Ulaya Mashariki wakati nchi nyingi tajiri za Ulaya zilikuwa Magharibi? Isipokuwa Finland, hakuna nchi za Kiskandinavia zilizoshambuliwa kwa lengo la kupanua eneo. Uvamizi wa Ujerumani katika nchi ya Norway ulikusudiwa kwanza kwa ajili ya kuzuia uvamizi wa Uingereza (Ziemke, 1990). Miongoni mwa wapiganaji wakubwa hakuna yeyote aliyesukumwa na shauku ya kuteka Norway au kupata eneo la nyongeza au raslimali kwa nguvu. Uvamizi uliopangwa wa Uingereza – Ufaransa ulikusudiwa kulinda njia za meli za kaskazini na malengo ambayo yalikuwa na maana kufanya vita kubwa. Hakika, hali ya Norway kutokufungamana na yeyote ilielekea kukamilisha malengo ya Ujerumani4. Hitler hajawahi kushambulia Sweden yenye utajiri mkubwa na chanzo kikubwa cha Wajerumani cha mawe yenye madini ya chuma, ambayo nusu yake ilisafirishwa kupitia Norway (Fox, 1959; Hägglöf, 1960)5. Hata baada ya marafiki kushindwa kuingilia kati, Ujerumani ilipendelea kununua, kuliko kuchukua kwa kutumia nguvu, mali nyingi ya rasi ya Scandinavia6.

Hii haimaanishi kwamba Sweden haikuathiriwa na vita. Maofisa wa Nazi walitumia kutokulingana huko katika nguvu kuishinikiza serikali ya Sweden kuhusu masuala mbalimbali, hususan upitishaji wa vifaa na wafanyakazi kupitia nchi ambayo haifungamani na yoyote. Sweden ilibakia huru kwa kuwa ilizalisha zaidi kupeleka Axis kwa kutumia biashara kuliko uvamizi na kwa sababu iliamuliwa kwa busara kuegemea kidiplomasia pale ambapo Norway iliacha (Carlgren, 1977)7. Bado, Ujerumani ilichagua kutokuvamia Sweden wakati ingeweza kufanya hivyo kwa urahisi. Uwezo wa kujizuia wa Hitler kwa kiasi kidogo sana ulisababishwa na upinzani au vikwazo vya kimaadili katika kutumia nguvu ya uhuru. Badala yake inaonyesha kuwa makisio mepesi kung’amua hayo yalifanywa kwamba ilikuwa rahisi kufanya biashara kuliko kuchukua raslimali zilizohitajika za Sweden.

Mchakato wa pili Angell anaouonyesha unahusisha ulegezaji wa masharti ya kiuchumi. Kuongezeka kwa ushirikiano wa masoko ya dunia kunarahisisha upataji wa bidhaa na huduma kupitia biashara na ugumu kuepuka wawekezaji wasio na utulivu katika vita. Angell anafikiria Jeshi la uvamizi la Ujerumani mjini London.

Pamoja na manufaa ambayo Ujerumani ingeweza kupata kwa kushikilia dhahabu ya Uingereza, hakika, ingekuwa zaidi ya fidia kwa ukweli kwamba lilikuwa tendo la kikatili la serikali ya Wajerumani ambalo limesababisha balaa kubwa. Nchi ambayo ingeweza kupora akiba ya benki ingefaa kuepukwa na wawekezaji: umuhimu wa mkopo ni imani, na wale ambao

wanakataa kuulipa wanalipia vitendo vyao. Jemadari mkuu wa majeshi yote ya Kijerumani mjini London anaweza asiwe na ustaarabu zaidi ya Anlaf mwenyewe, lakini karibuni angeona tofauti baina yake na Anlaf. Anlaf hakupaswa kuona shaka kuhusu kiwango cha benki na matatizo kama hayo; lakini Generali wa Kijerumani, akijaribu kupora Benki ya Uingereza, anaweza kukuta salio lake mwenyewe kwenye Benki ya Ujerumani limetoweka, na thamani ya hata sehemu kubwa ya vitega uchumi vyake imepungua. (Angell, 1933:106-07).

Kwa mara nyingine tena Angell ameonekana kukosea, labda mtu aangalie kwa karibu sana. Mara kwa mara, inakumbukwa kwamba Vita Kuu vya Kwanza vya Dunia vilianzia Balkans lakini kwa ujumla inasahaulika kwamba Balkans ilikuwa sehemu iliyokuwa ya nyuma sana kiuchumi katika Ulaya. Wakati vita haikuwepo katika mfululizo wa migogoro miongoni mwa mataifa makubwa ya Magharibi yaliyotegemeana kiuchumi hadi 1914, migogoro katika Balkans kila wakati ilipelekea kwenye vita (Strachan, 2001). Hivyo, mgogoro katika Balkans ni rahisi kuielezea kwa kuangalia uhuru wa kiuchumi. Mashindano ya ndani yaliyoanzishwa na Austria – Hungary dhidi ya Serbia yalienea katika mfumo mkubwa wa ushirikiano wa marafiki (Kissinger, 1994)8. Tatizo la Ulaya kwa 1914 lilikuwa hasa kwamba ulegezaji masharti ya uchumi na ushirikiano wa kiuchumi havikuwa sawa, wakati wajibu wa kisiasa ulihakikisha kuwa kutegemeana kiuchumi huko Magharibi hakukuwa na maana tena.

Mataifa yaliyoendelea sana yalifanya sera zao za nje kuwaza kibalkan ili kuongeza nguvu ya ushawishi ya kujadiliana malipo ya mataifa yenye nguvu ya Ulaya Mashariki. Kwa kiwango kwamba uhusiano wa kirafiki uliheshimiwa, maamuzi ya uhamasishaji yalikuwa mikononi mwa nchi hizo ambazo hazikutegemea vizuizi vya kiuchumi ambavyo Angell alielezea kwa ushawishi mkubwa.

Kushindwa kutegemeana kiuchumi katika kuzuia uenezaji wa mawazo potofu ya vita hakumaanishi kutokufaa katika kuzuia cheche za awali. Kushindwa kutabiri vita ya dunia kulifunika ukweli muhimu wa madai ya Angell. Matukio yaliyofuatia vita yalionekana kulingana na dira ya Anglii ya amani isiyo na upendeleo. Uchumi wa sasa hauonekani kama unaongozwa na uvamizi wa kijeshi (Brooks, 1999)9. Hivyo, kosa la Angell ni kwamba anatoa dhana finyu kupita kiasi ya sababu za mgogoro kati ya nchi na nchi. Nchi zinashindana, sio kwa ajili ya raslimali, bali juu ya sera na jiografia mkakati. Mtu anapokaa kwenye ramani ina maana maalum, hususan kama yuko baina ya wahusika wakuu katika migogoro (Fazal, 2002). Vivyo hivyo kinachotakiwa na nchi, bila kutegemea thamani ya maeneo au raslimali zake, kinaelekea kuvuta vivutio vya wengine ili kulaumu au kuzipeleka vitani (Maravcsik, 1997). Hivyo, amani ya kibepari inayoahidiwa na Angell na kundi lingine la kimapokeo sio mbaya bali haijakamilika. Maelezo kama yalivyoendelezwa yana utambuzi muhimu kwamba, mara yatakapopitiwa, yatathibitisha kwamba ni nadharia jarabati, halali.

Amani ya Kibepari
Maelezo Yanayoendelea

Katika Msimamo wa Kisheria, Montesquieu anasema kwamba “Mfanyabiashara tajiri sana alikuwa tu na mali isiyoonekana ambayo ingeweza kupelekewa kila mahali bila ya kuacha hata kiasi kidogo… [ili] watawala wamelazimika kutawala kwa hekima nyingi sana kuliko ambavyo wenyewe wangeweza kufikiri” (1989 [1748]: 389). Uhuru wa kiuchumi maana yake unaweza ukauchukua. Wakati hali ikiwa mbaya ndani, mtaji huweza kuondoka nchini, na kutengeneza ukame kiuchumi na hivyo kisiasa katika jamii. Ni wazi kwamba, serikali hazitaki fedha zitoke. Kwa kiwango ambacho watawala hawawezi kuzuia kuondoka kwa mtaji, hata hivyo, lazima watengeneze mazingira yatakayosaidia uwekaji wa fedha kwa hiari ndani ya mipaka yao.

Utamaduni wa wasomi wanaopenda mabadiliko ya amani katika uchumi yaliyoanza na Montesqueieu, Mill, Adam Smith, na wengine, na kuendelea hadi kwa Richard Cobden, Norman Angell, na Richard Rosecrance inaweza kuhimiza amani. Labda maelezo ya jumla zaidi ni kwamba kutegemeana kiuchumi kunaweza kuleta kitu cha thamani ya pamoja kwa nchi, kuziacha nchi kukataa kufanya kitu kupambana kwa ajili ya hofu ya kuharibu manufaa ya uchumi wanaouthamini sana.

Wakati haya ni kweli, maelezo yanategemea kufikiria kwamba vipengele vya thamani ya pamoja vyenyewe havianzishi wala kuwezesha mgogoro. Thomas Schelling anaeleza hadithi ya wapanda mlima wawili waliofungwa pamoja na kamba ambayo husababisha pamoja na kamba ambayo husababisha waelekee sehemu moja. Schelling anaonyesha namna kitu chenye thamani kwa wote kinavyoweza kutumika kimkakati kumtawala mwenzie; nchi ambazo zina ushirikiano wa kiuchumi zinaweza kucheza mchezo wa kuku: uhusiano ulivyo mkubwa sana, mchezo ndio unafanikiwa na kuelezeka (Schelling, 1966: 99-100). Kama nchi inasita kuhatarisha faida za uhusiano wa uchumi unaostawi, sio kwamba amani itafuatia. Nchi nyingine zinaweza kushawishika kutazama usitaji wa kupigana kama kuweza kudhuriwa. Ili kuhakikisha kuna amani, washiriki wote lazima wasiwe tayari kucheza mchezo wa kuku au, hakika, kutumia nguvu za kijeshi.

Zamani wanafunzi wa ushirikiano wa kimataifa waliangalia sababu na fursa za kuelezea vita. Hata hivyo, kama ilivyo kwa vitabu vya hadithi za mauaji ya siri na mchezo wa Clue unaoweka wazi, masharti haya mara chache hutosha. Watu binafsi, vikundi, na nchi mara nyingi zinakataa, bali kwa kawaida vyombo vyenye raghaba tofauti vinajikuta vinaweza kujadiliana bei ambazo zinaweza kuepuka gharama zaidi au tabia za ushaufu. Nini sasa kinachoelezea kufanikiwa au kushindwa kidiplomasia?

Mojawapo ya matatizo ya msingi katika ushirikiano wa kimataifa – ni kufahamu wakati mpinzani anapokuwa anasema au hasemi ukweli. Viongozi wakati wote watadai kuwa tayari kutumia nguvu wakati ukweli ni kwamba wanadanganya. Vita hutokana na sababu kadhaa lakini kinachochangia hasa ni kutokuwa na uhakika kuhusu mapatano ya dau ambalo lingekubaliwa na mpinzani. Kama mtu anakubali kuwa vita ni mbinu ambayo ina gharama kubwa ya kuamua umiliki wa raslimali au haki za sera, kisha ziada

inayotokana na ufumbuzi wa kidiplomasia inapaswa kufanya majadiliano ya kupatana bei kupendelea kupigana10.

Kama wachezaji wa poka wanavyolinda kazi zao, uongozi wa kisiasa wa mataifa unaona kwamba wakati mwingine unapaswa kudanganya ili kushinda. Kwa kutokuwa na uhakika na vichocheo vya kudanganya, hata hivyo, diplomasia inaweza kushindwa na migogoro kuzuka. Baada ya hapo vita hufichua maelezo kuhusu "kadi" zilizoshikiliwa na wapiganaji husika (taarifa kuhusu uwezo wianifu wa nchi na ufumbuzi). Kwa hakika, ili vita ikome, pande husika katika mashindano lazima zijifunze kwa kiasi cha kutosha kufanya mapatano kuhusu majadiliano ya malipo ya pamoja yaliyokubalika. Uhuru wa kiuchumi ni muhimu kwa amani kwa angalau sababu mbili. Kwanza, masoko huria hufanya kazi kama njia ya kuenezea maoni kwa ajili ya shughuli za kisiasa. Vitendo vinavyotishia masoko vinapinga uwekezaji, kushusha chini masharti ya uchumi wa ndani, na hivyo yanaelekea kuepukwa na viongozi wa ndani. Utumiaji wa nguvu ng'ambo mara nyingi unahusishwa na kushuka kwa uwekezaji wa ndani na mbubujiko wa mtaji (Bueno de Mesquita, 1990). Kwa kiwango kwamba viongozi wako tayari kutoa matamko ya sera ya nje ambayo yanatishia masoko ya mtaji, na kwa kiasi kwamba sera hizo huru za fedha zipo ambazo zinaleta ugumu kwa serikali kuingilia mtiririko wa mtaji, jumuiya ya kimataifa inaweza kuona azma ya kweli ya viongozi. Kwa kujua kile ambacho mpinzani yuko tayari kufanya kunasaidia kujadili malipo kwa ufanisi zaidi, ili kwamba kukimbilia kufanya vurugu ili kupata kile ambacho upande mmoja unahitaji mara nyingi sio lazima sana. Masoko huru ya kuleta kuaminika bila ya kuhitaji kushadidia nguvu ya kijeshi (Gartzke na wenzake, 2001; Gartzke & Li, 2003).

Jedwali la 2.1 linabainisha viukilia vya migogoro ya kijeshi kati ya nchi na nchi (MIDS), inayoelezewa kama tishio kubwa sana au utumiaji mkubwa wa nguvu, hadi kufikia na kujumuisha vita vinavyohusisha vifo 1000 kwenye uwanja wa vita. MIDS ni kiashirio kikubwa cha tabia ya migogoro kinachotumiwa na watafiti katika ushirikiano wa kimataifa (Gochman na Maoz, 1984, n.k) yamewekwa alama ya "1" kama kuna mgogoro katika mwaka huo unaohusu nchi na "0" vinginevyo. Uchambuzi wa kurudi nyuma unaleta kizigeu kati ya vipimo viwili kwa kila chenye kubadilikabadilika, ambao unaonyesha ukubwa wa athari wa kitu hicho kinachobadilikabadilika kuhusu uwezekano wa kuwepo kwa MID hapo kwa mwaka husika, kwa kuzingatia athari ya vitu vingine vinavyobadilikabadilika.

Mkadiriaji wa kurudi nyuma pia anaonyesha jinsi mtu anavyopaswa kujiamini katika kizigeu wiano kilichokadiriwa. Matukio ya kijamii kwa kawaida huonekana kama yenye welekeo: hata wakati vipengele vyote muhimu vinavyochangia vinafanana, matokeo yanaweza kutofautiana kutoka jambo hadi jambo. Labda uhusiano ulio dhahiri baina ya kitu huru kinachobadilikabadilika na migogoro ni dhahiri tu. Mfano wa kurudi nyuma unashughulikia tatizo hili kwa kuanzisha safu au mgawanyo wa uhusiano unaowezekana baina ya chanzo na athari. Kosa kubwa linaonyesha "kuenea" kwa mgawanyo huu wa kizigeu kinachowezekana.

Kama kosa ni kubwa likilinganishwa na kizigeu (takribani, kubwa zaidi ya nusu ya ukubwa wa kizigeu), basi inawezekana kuwa kizigeu halisi kinachozalisha data ni sawa na ziro na kwamba

hakuna uhusiano uliopo baina ya kitu kinachobadilikabadilika na iwapo nchi zinapigana. Kipimo cha “umuhimu wa kitakwimu” kinachonyesha kitu ambacho tungeweza kukubali bila usahihi wa kizigeu kama kinavyoonyesha uhusiano baina ya chanzo na sababu. Ubadilishaji ni kutumia kiwango muhimu cha juu cha 1%, 5%, au 10%. Ili kukubali uhusiano, tunahitaji kwamba kati ya majaribio 100 yenye data zinazolingana, kati ya 90 na 99 ya makadirio ya kizigeu kilichotolewa ziwe tofauti kutoka ziro13.

Jedwali la 2.1 Athari ya Uhuru wa Kiuchumi kwenye Migogoro ya Kijeshi Kati ya Nchi (MIDs)

| Nyanja | Kizigeu | (Kosa) |
|---|---|---|
| Uhuru wa kiuchumi | -0.567** | (0.179) |
| Uwezo | 2.777 | (8.491) |
| Idadi ya watu | 2.08×10-6* | (8.18×10-7) |
| Nguvu kubwa? | 0.853 | (1.133) |
| Alama za Demokrasia | -0.628 | (0.065) |
| Mkataba wa ulinzi? | -0.011 | (0.482) |
| GDP kwa kila mtu | 8.01×10-6 | (8.04×10-5) |
| Uwazi wa Biashara | 1.57×10-7 | (1.50×10-6) |
| – Spline 1 | 6.08×10-4** | (2.32×10-4) |
| – Spline 2 | -4.53×10-4* | (1.76×10-4) |
| – Spline 3 | 1.19×10-4* | (4.48×10-5) |
| Kuingilia kati | -0.381 | (1.210) |
| | | |
| N | 2519 | |
| Log – Likelihood | -161.719 | |
| X2(II) | 160.564 | |

Viwango muhimu +: 10% *:5% **:1%

Mkabala huu unathibitisha kwamba dunia ina mshindo mkubwa ("stochastic") wakati huohuo kupunguza hatari ya kukubali nadharia ambazo kwa hakika ni za Uongo. Chanzo kikuu au vitu "pekee" vinavyobadilikabadilika katika uchambuzi ni uhuru wa kiuchumi. Hiki ni kielelezo kilichotengenezwa na Gwartney, Lowason na wengineo kupima msimamo wa kupendelea mabadiliko wa uchumi wa nchi. Kama inavyoweza kuonekana katika Jedwali la 2.1, uhuru wa kiuchumi kipekee hupunguza uwezekano wa nchi kuwa na mgogoro14. Vipo vipengele vingine kadhaa vinavyobadilikabadilika vilivyoingizwa kwenye uchambuzi ili kuhakikisha kuwa matokeo kwa ajili ya uhuru wa kiuchumi sio ya uwongo. Vipengele hivi vyote vinavyobadilikabadilika ni vya kawaida sana katika utafiti wa kiasi wa migogoro ya kimataifa. Uwezo unajaribu kushika dhana ya "nguvu" kwa kuripoti asilimia ya wastani ya uwezo wa jumla wa dunia mbao taifa linaweza kuwa nao katika makundi sita yanayoonyesha vipengele vinavyobadilikabadilika vya kijeshi, kiuchumi na kidemografia. Nchi kubwa na zenye nguvu zinaelekea kuwa na migogoro zaidi kuliko zile ndogo. Idadi ya watu inaripoti jumla ya idadi ya watu wazima kwa nchi. Alama ya Demokrasia ni kiashirio cha kiasi cha "udemokrasia" cha nchi. Nguvu kubwa? Na Mkataba wa Ulinzi? Ni vipengele vinavyobadilikabadilika vya mwainisho wenye upinzani (mwigo) vilivyopewa alama "1" kama nchi husika ni nguvu kubwa au kama nchi ina urafiki mkubwa kijeshi na nchi nyingine ambayo inaweza kuusaidia wakati wa vita. Pata Ghafi la Taifa kwa kila mtu linapima wastani wa pato la taifa nchini. Hili ni muhimu kujumuisha, kwa kuwa tunatafuta kujua kama ni ustawi wenyewe au kwa ufinyu ziadi uhuru wa kiuchumi ambao uHoja za Uongobisha amani. Vivyo hivyo, Uwazi wa Biashara unaweza kuwa ni kitu kingine kinachozuia migogoro. Mwishowe, ninajumuisha idadi ya vipengele vinavyobadilikabadilika ambavyo vinashughulikia tatizo la kiutaalamu linalotokea wakati tabia ya vita inahusishwa na jinsi wakati unavyokwenda. Mbinu ya ukadiriaji hudhania kwamba migogoro haihusiani. Ni wazi, mgogoro katika mwaka husika unaweza kuenea na kuchangia kwa mingine inayofuatia. Kuongoza vipengele vinavyobadilikabadilika vya spline kunahakikisha kwamba matokeo hayatokani na chanzo cha usababisho15.

Mbele ya vipengele vinavyobadilikabadilika vya spline, ni Uhuru wa Kiuchumi tu na, pili, idadi ya watu ndiyo muhimu kitakwimu. Muundo wa uchumi na kwa kiwango fulani ukubwa wa kidemografia huathiri migogoro lakini hatuwezi kutumaini kwamba vipengele vingine vinavyobadilikabadilika vina athari kuhusu kama nchi inapigana.

Wakati mtu anaweza kuangalia kizigeu na makosa ya kiasi kwenye Jedwali la 2.1 na haraka kuamua iwapo uhusiano unaodaiwa unafaa kukubaliwa (au usikataliwe), ni rahisi kidogo kuamua ni kiasi gani kipengele kinachobadilikabadilika kinafaa kama nchi zinapigana. Kurudi nyuma kilogitii kunaruhusu watafiti kuchunguza hali iwapo matokeo ya raghaba ni ya mwainisho wenye ukinzani (k.v. "vita", "hakuna vita"). Hata hivyo, kwa sababu za kiufundi, mkadiriaji wa kurudi nyuma lazima ayashughulikie matokeo kama vile yalikuwa yanaendelea (k.v. kwa kadri ya kitu, kama vile kukadiria ukubwa au uelekeo wa mgogoro), Badala ya kutabiri kuwepo kwa mgogoro au kutokuwepo kwa mgogoro, kisha, mkadiriaji wa logiti anatabiri uelekeo wa kuwepo

na ugomvi. Ili kuhakikisha kuna raslimali nzuri kwa ajili ya uelekeo uliotabiriwa, logiti inatumia uwiano unaohusu batli asilia16. Kama vile kubadilisha viwango vya desimali kwa mfumo wa alama wa jozi ili kuviruhusu vitathminiwe na kompyuta, kigeuzi cha logi kinawezesha makadirio na majaribio muhimu kwa kiasi cha gharama ya kuhisi. Vizigeu vinavyotokea vinafafanuliwa vizuri zaidi kwa uwekaji uelekeo uliotabiriwa unaokadiriwa na kurudi nyuma kwa logiti.

Athari halisi za Uhuru wa Kiuchumi na Alama za Kidemokrasia kuhusiana na migogoro ya kimataifa zinaweza kuonekana katika mchoro 2.1 na 2.2, mtawalia. Katika michoro yote miwili, mhimili wa mlalo unaorodhesha vipimo vya mpango kwa ajili ya vipengele husika vinavyobadilikabadilika (ama Kielelezo cha Uhuru wa Kiuchumi au kielelezo cha serikali ya Kidemokrasia), wakati mhimili wa wima unaripoti uelekeo wa MID katika mwaka husika kwa nchi zenye kiwango cha mojawapo ya vipengele viwili vinavyobadilikabadilika vinavyojieleza. Mstari mnene unaoinama chini kuelekea kulia katika Mchoro wa 2.1 ni uhusiano baina ya Uhuru wa Kiuchumi na migogoro ya kijeshi, kama ilivyokadiriwa kwa kurudi nyuma katika Jedwali la 2.1. Katika Mchoro wa 2.2, athari ya Kipengele kinachobadilikabadilika cha Alama ya Kidemokrasia kuhusu mgogoro huonyesha pia kama mstari mnene, unaoinama chini kidogo na kuelekea kulia. Katika mchoro wa 2.1, mistari miwili ya dashi hafifu ambayo inaonekana kwenda uhuru wa kiuichumi inawakilisha vipindi vya kujiamini. Asilimia tisini na tano ya mistari yote minene iliyokadiriwa kutoka kurudi nyuma kwa data zinazofanana ingekuwemo ndani ya kipindi kilichopakana na mistari miwili yenye dashi. Kwa maneno mengine, uhusiano ulioonyeshwa katika mchoro baina ya Uhuru wa Kiuchumi na kutokuwepo na vurugu za kijeshi unaelekea angalau kuwa sahihi.

Kama inavyoweza kuonekana katika serikali yenye upungufu ni makubwa. Nchi huru ndogo zaidi zina karibu nafasi ya 7% ya kuwa na migogoro, wakati nchi zilizo huru zaidi huwa na migogoro kwa karibu nusu tu ya 1% ya mwaka uliochunguzwa. Kuufanya uchumi kuwa huru zaidi maana yake ni kuzifanya nchi kuwa na amani zaidi. Kwa kuzidi sana, nchi zilizo huru kidogo ni karibu mara 14 kuwa na migogoro kama zilizo huru zaidi.

Hayohayo hayawezi kusemwa kwa uhusiano baina ya demokrasia na mgogoro. Nafasi ya mlalo ya mstari katika Mchoro 2.2 inaonyesha kuwa kipengele kinachobadilikabadilika cha Alama ya Kidemokrasia hakina athari kwa migogoro ya kijeshi.17 Nchi zenye demokrasia ndogo (karibu ziro) na zenye demokrasia kubwa (karibu 10) zinaelekea zaidi kuwa na migogoro. Ukweli ni kwamba, mlingano wa kiwango cha kuzidi sana wa Uhuru wa Kiuchumi wa Alama ya Kidemokrasia unaonyesha kwamba aliyetangulia ana takriban mara 54 zaidi ya athari kuhusu tabia ya mgogoro kama wa kwanza.

Wala mtu asichukue ukweli kwamba mstari wa Alama za Kidemokrasia ni karibu na Ziro kama ishara kwamba vita haviwezi kutokea katika demokrasia. Uamuzi hutegemea mabadiliko ya pande zote. Bila ya kujali kama mbinu ni za asili (za majaribio), kinadharia, au kitakwimu, mtu "anatafutiza" chanzo na kutazama mwendo unaohusiana katika kipengele kinachobadilikabadilika cha matokeo. Hapa hakuna mwendo katika matokeo; demokrasia haiathiri welekeo wa MIDs. Ukweli kwamba viwango vya juu vya kipengele

kinachobadilikabadilika cha Alama za Kidemokrasia kinaongeza migogoro. Mstari wa mbele juu ya ule wa chini katika Mchoro 2.2, mstari wa dashi hafifu kwa kipindi cha juu cha imani, uhusiano uliokadiriwa katika data zinazofanana vitatoa ripoti kwamba demokrasia hufanya migogoro iweze kuwepo.

Vipengele vya ziada vinavyozingatiwa

Vipengele viwili vya uthibitisho vimetumika kuelezea amani katika zama za sasa ambavyo havikujumuishwa kwenye uchambuzi katika Jedwali 2.1. Kwanza, baadhi ya nchi zimo kwenye mipangilio ya pamoja ya usalama au mipangilio ya biashara ya kanda ambayo inaweza kupunguza tabia ya kupigana wenyewe kwa wenyewe. Umoja wa Ulaya (EU) labda ni mfano bora zaidi wa jumuiya ya mataifa ambayo inafikiriwa kubadili vita kwa mafanikio kwa mwingiliano wa amani. Sababu zinatofautiana bali wengi wamedai kwamba asasi na utamaduni wa EU vinahimiza fikra na kuzuia vurugu miongoni mwa wanachama. Pili, watafiti kama vile Kenneth Waltz na John Mearsheimer wanasisitiza kwamba silaha za nyuklia zinaweza kuwa kama kizuizi. Nchi zinaweza kusita kupigana na nchi zenye silaha za nyuklia. Ili ujaribu vipengele hivi vinavyowezekana vya kustaajabisha sana, ninaongeza vipengele viwili vinavyobadilikabadilika ambavyo vinapima uanachama katika Jumuiya ya Ulaya na umiliki wa silaha za nyuklia katika Jedwali la 2.2. Mwanachama wa EU? ni kipengele kinachobadilikabadilika mwigo sawa na “1” kama nchi ni mwanachama wa Jumuiya ya Ulaya katika mwaka husika. Vivyo hivyo, Silaha za Nyuklia? hubainisha zile nchi zilizomiliki, au ambazo ziliaminika pote kwamba zilimiliki, silaha za nyuklia katika mwaka husika. Wala kipengele kinachobadilikabadilika hakitabadilisha kwa kiasi kikubwa welekeo kwamba nchi itahusika katika mgogoro wa kijeshi. Zaidi ya hayo, uhuru wa kiuchumi unabakia kuwa mtabiri muhimu kitakwimu wa tabia ya migogoro.

Ni muhimu kuhakikisha kwamba matokeo yaliyoripotiwa hapa hayatokani na kosa au mawazo ya kutamani. Uchunguzi wa maelezo mbadala yanayowezekana yasingeonekana kikamilifu kama tungepuuza vipengele vinavyobadilikabadilika vya kidemografia. Vipengele vya kidemografia vinavyowezekana ni vingi. Nimechunguza vingi lakini nitatoa mifano michache tu katika Jedwali la 2.3. Eneo la Ardhi la Jumla linaripoti idadi ya hektari za ardhi lililozungukwa na mipaka ya nchi. Kijiografia nchi kubwa sana, bila ya kuangalia idadi ya watu, zinaweza kufanya mambo tofauti na nchi ndogo, ambazo nyingi hutegemea biashara zaidi. Inawezekana pia kwamba nchi zenye watu wengi sana huwa na migogoro sana. Msongamano wa idadi ya watu unaonyesha idadi ya watu wazima kwa hektari, yawezekana unaakisi “Shinikizo la pembeni” (Choucri na North, 1975, 1989). Idadi ya Nchi Enezi zinaonyesha iwapo nchi ina majirani wengi na kwa hiyo kuwa na uwezekano wa migogoro mingi. Hatimaye, Ardhi Inayolimika/Idadi ya Watu inatofautisha nchi zenye maeneo makubwa ya makazi na malisho na zile zenye ardhi kubwa ya kilimo. Kama mwanzo, hakuna badiliko katika matokeo kwa kipingele kinachobadilikabadilika cha Uhuru wa Kiuchumi na hakuna kimojawapo kati ya vipengele vinavyobadilikabadilika vipya ni muhimu kitakwimu.

Jaribio la mwisho la nguvu linahusisha kugawa sampuli ya nchi kwa kanda. Utafiti wa hivi karibu wa ushirikiano wa kimataifa umesisitiza umuhimu wa utofauti wa kanda. Tabia ya migogoro ya nchi za Afrika husababishwa kwa sehemu na vipengele tofauti na vile vinavyosababisha tabia za migogoro huko Ulaya au Amerika Kaskazini. Ili kushughulikia uwezekano kwamba matokeo ya Uhuru wa Kiuchumi yanaweza kuakisi tofauti za kikanda, ninajumuisha seti ya vipengele vinavyobadilikabadilika mwigo katika kanda. Vipengele hivi vinavyobadilikabadilika vilivyowekwa alama kwa ajili ya kanda husika18 vimeongezwa kwenye Jedwali la 2.4. Baadhi ya miigo ya kikanda ni muhimu kitakwimu, kuonyesha kwamba vyanzo vya migogoro hutofautiana katika sehemu tofauti za dunia. Hata hivyo, Uhuru wa kiuchumi hausumbuliwi na kuwepo kwa kanda mbalimbali. Matokeo yanaonyesha uhusiano mkubwa zaidi baina ya masoko huria na amani. Hakika uhuru wa kiuchumi ni kipengele pekee kinachobadilikabadilika ambacho kinathibitisha ulinganifu kitakwimu na kiumuhimu katika michanganuo hii.

Mustakabali wa Amani ya Kibepari

Matokeo yaliyoripotiwa hapo juu yanawezesha kubahatisha kuhusu kuanza kwa ushirikiano wa kimataifa. Baadhi ya vidokezi vinaleta matumaini na baadhi havileti. Nchi zenye uchumi huria na unaostawi zina nafasi nzuri ya kudumisha na hata kuzidisha amani ambayo ilikuwepo kwa iliyotangulia kwa nusu ya karne ya ishirini kuhama.

Jedwali la 2.2: Kuongeza Uanachama katika EU na Umiliki wa Silaha za nyuklia

| Kipengele kinachobadilika<br>Badilika | Kizigeu | (Kosa kiasi) |
|---|---|---|
| Uhuru wa kiuchumi | -0.531** | (0.176) |
| Uwezo | 2.917 | (9.151) |
| Idadi ya watu | 1.68×10-6* | (9.74×10-7) |
| Nguvu kubwa? | 0.452 | (1.130) |
| Alama ya Demokrasia | -0.030 | (0.065) |
| Mkataba wa ulinzi? | -0.472 | (0.560) |
| GDP kwa kila mtu | 2.95×10-6 | (8.14×10-5) |

| | | |
|---|---|---|
| Uwazi wa Biashara | 4.43×10-7 | (1.46×10-6) |
| Uanachama wa EU? | -0.865 | (0.865) |
| Silaha ya Nyuklia? | 1.321 | (1.014) |
| – Spline 1 | 6.16×10-4** | (2.35×10-4) |
| – Spline 2 | -4.62×10-4** | (1.77×10-4) |
| – Spline 3 | 1.23×10-4* | (4.8×10-5) |
| Muingiliano | -0.562 | (1.341) |
| N | 2519 | |
| Log – Likelihood | -159.49 | |
| X2(I3) | 275.447 | |

Viwango vyenye umuhimu +: 10% *:5% **:1%.

Jedwali la 2.3 Uchunguzi wa sababu za ziada za

Kidemografia

| Nyanja | Kizigeu | (Kosa la kawaida) |
|---|---|---|
| Uhuru wa kiuchumi | -0.779** | (0.221) |
| Uwezo | 4.461 | (13.281) |

| | | |
|---|---|---|
| Idadi ya watu | 2.27×10-6* | (1.14×10-6) |
| Taifa kubwa? | 1.148 | (0.969) |
| Alama za Demokrasia | -0.008 | (0.0659) |
| Maafikiano ya Ulinzi? | -0.536 | (0.462) |
| GDP kwa kila mtu | 1.12×10-5 | (6.63×10-5) |
| Uwazi wa Kibiashara | 5.03×10-8 | (1.50×10-6) |
| Jumla ya Eneo la Ardhi | 8.74×10-8 | (1.69×10-7) |
| Wingi wa watu | 2.87×10-4 | (2.42×10-4) |
| Idadi ya Nchi za Jirani | -0.157 | (0.097) |
| Ardhi inayolimika/idadi ya watu | -0.23 | (0.111) |
| – Spline 1 | | |